

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 29 Januari, 2013

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA

(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa kabla ya kuanza Kikao cha Bunge)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu kikao cha mwisho cha Bunge uliopita.

MASWALI NA MAJIBU

Na.1

Baadhi ya Vijiji vya Mwibara Kukosa Zahanati

MHE. MWIGULU L. N. MADELU (K.n.y. MHE. KANGI A. LUGOLA) aliuliza:-

Baadhi ya Majimbo hapa nchini yana Zahanati kwa kila Kijiji wakati Jimbo la Mwibara na Vijiji vyake 36 havina Zahanati:-

Je, ni vigezo gani vimetumika kujenga Zahanati hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa Niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upangaji wa Mipango ya Maendeleo katika Halmashauri unaanzia katika ngazi ya Kijiji, kwa kuzingatia Mpango Shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (*O & OD*). Kupitia mfumo huu, Wananchi wanaibua Miradi ya Maendeleo kwa kuzingatia aina ya matatizo yaliyopo. Aidha, Wananchi wanashiriki pia katika utekelezaji wa Miradi hiyo kwa

kuchangia nguvu kazi. Halmashauri inachangia pale uwezo unaporuhusu ili kuhamasisha nguvu ya Wananchi. Vilevile moja ya majukumu ya Mfuko ni kuchochaea maendeleo katika Jimbo hilo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina Vijiji 106. Kati ya Vijiji hivyo ni Vijiji 33 tu ndiyo vyenye Zahanati 22 katika Jimbo la Bunda na Zahanati 11 katika Jimbo la Mwibara. Hivyo, Vijiji ambavyo havina Zahanati katika Jimbo la Mwibara ni 37 na Vijiji 36 havina Zahanati katika Jimbo la Bunda.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri inaendelea na Ujenzi wa Vituo viwili vya Afya vya Kasuguti na Kisorya. Aidha, Halmashauri katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2012/13, imetenga shilingi milioni 300 kupitia Fedha ya Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (*LGCDG*), kwa ajili ya ujenzi wa Zahanati katika Vijiji vinne vya Neruma, Mwitende Namalebe na Namalama, ambavyo viko katika Jimbo la Mwibara. Aidha, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), zimetengwa shilingi milioni 35 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya. Utekelezaji unafanyika, jumla ya shilingi milioni 300 zimetengwa kupitia *LGCDG* na shilingi milioni 35 zimetengwa kupitia MMAM.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri, kwa kutambua jitihada za Wananchi katika kuongeza nguvu kazi, kujenga Vituo vya Afya na Zahanati. Katika maeneo mengi Wananchi walihamasika sana wakatoa nguvu kazi zao na wakajenga maboma kama ilivyokuwa agizo la Serikali lakini sehemu iliyosalia ambayo ilitakiwa ikamilishwe na Serikali katika vituo vingi haijakkalimishwa. Nini kauli ya Serikali kwenye hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kama anavyosema Mheshimiwa Mchemba ni kweli kabisa kuwa, kazi kubwa imefanywa na wananchi na ni kweli kuwa kuna maeneo mengi ambayo hayajamalizika kwa sababu kama tuliyoeleza hapa ni kuwa, kazi hii inafanywa na wote, yaani Wananchi, Halmashauri pamoja na Serikali wote tunashirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunawapongeza Wananchi kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika Halmashauri zetu, kwa sababu wameitikia wito wa Serikali kwamba kila Kijiji walau kiwe na Zahananti moja na Kata iwe na Kituo cha Afya na Hospitali. Maelekezo yetu sisi kwa Halmashauri ni pale ambapo nguvu za Wananchi zimejitokeza kiasi hicho kama inavyosemwa hapa, basi mwishoni pale kuna *element* ya Halmashauri kupeleka nguvu kidogo ili kuhamasisha.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tumetaja hela za *Constituency Development Catalyst Fund*, ambazo zinapita kwa Wabunge, ambazo moja ya kazi ni kusaidia gharama pale. Ndicho tunachowenza kusema kwa sasa hivi, lakini tunapongeza kazi nzuri ambazo zinafanyika na tunaziagiza Halmashauri popote pale ambapo inaonekana nguvu za Wananchi zimejitokeza kama ilivyojitokeza hapa, basi na Halmashauri ziweze ku-*chip in* na kusaidia.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri kama ifutavyo:-

Maeneo mengi katika Majimbo ya Kilwa Kaskazini na hapa nchini, Wananchi wamekuwa wakifanya jitihada za kujenga majengo na kuyakamilisha, lakini vifaa tiba na wahudumu wa afya ni matatizo kama ilivyo katika eneo la Zinga, Miumbu na Nambondo. Nini mkakati wa Serikali kupeleka vifaa tiba, Wahudumu wa Afya na Waganga katika hospitali hizi ili jitihada zilizofanywa na Wananchi zizae matunda waliyokusudia?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa tunayo matatizo anayoyasema na kwamba, *demand* sasa inaonekana ni kubwa, kwa hiyo tunahitaji Madaktari zaidi, tunahitaji Wauguzi zaidi na hivi vifaa tiba pia tunavihitaji. Kwa kuanzia, ambacho kimefanyika sasa hivi, sisi tunafanya kazi na Wizara ya Afya, wapo wanaskia nikijibu hapa tunashirikiana. Moja ni kwamba, idadi ya wanafunzi ambao wanakwenda katika vyuo vyetu ni kubwa. La pili, tumeweka utaratibu kuwa kutoka sasa badala ya kuwapitishia TAMISEMI hawa Wauguzi na Madaktari, wapelekwe kule katika Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mimi nimetoka Mikoani, nimetoka Mpanda, tatizo tulilonalo ni kwamba, watumishi wengi ambao wanapangwa katika maeneo ya pembezoni, unakuta hawaripoti kule. Kwa hiyo, tumeanza kuzungumza kuangalia namna tutakavyoweza kuwashamasisha na kutoa motisha waweze kusaidia katika vituo hivi.

Mheshimiwa Spika, la pili, anazungumzia kuhusu vifaa tiba; hivi ni sehemu ya ile habari tunayoita *Community Health Fund (CHF)*. Kazi kubwa ni kusaidia ile ruzuku ya Serikali inayokwenda pale na katika Halmashauri nyingi tulizokwenda, tumekuta hela hizi wala ile *Community Health Fund* haipo, watu wanakwenda kwa ile inayoitwa papo kwa papo, yaani wanalipwa pale halafu wanatibiwa. Kwa hiyo, tumeihamasisha Halmashauri na Mkakati tunaofanya sasa ni kuhakikisha kuwa, watu wote wanajunga na Mfuko wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, kwa kumalizia wanapata shilingi milioni 250 kama mfano, ambapo Serikali inawaongezea kutoka *NHIF* shilingi 250, unakuta wana milioni 500. Katika mazingira ya namna hiyo, hutegemei tena kwamba, hivi vifaa vitakuwa vinakosekana na rai yetu ni kwamba, sisi sote na Mbunge wa Rombo ananisikia nikisema hivyo, kuwa tunawapongeza Watu wa Rombo kwa kufanya vizuri na hawana matatizo ya namna hii.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata, Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, atauliza swali hilo, kwa niaba yake ni Mheshimiwa Mchungaji Natse.

Na. 2

Mfumo wa Udhiliti wa Makusanyo ya Ushuru

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE (K.n.y. MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali hajjaweka mfumo wa ukaguzi wa udhibitit wa makusanyo ya ushuru katika vitega uchumi mbalimbali kama vile vituo vya mabasi ya abiria, masoko, maegesho ya magari na kadhalika; inapoteza mapato mengi kwa kutoa zabuni kwa makampuni binafsi kukusanya ushuru katika maeneo hayo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaweka mfumo wa ukaguzi na udhibitit wa makusanyo ya ushuru katika maeneo hayo?

(b) Je, kwa nini Serikali isitumie mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)* ili kuhakikisha kwamba nayo inashiriki katika kusimamia uchumi wake?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
(TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu na kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, ninaomba kutoa maelezo ya ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukusanyaji wa kodi na ushuru mbalimbali katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa unafanya kwa kuzingatia kifungu cha 13(1) – (6) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya Mwaka 1982. Kwa mujibu wa kifungu cha 26(1) na (2)(a) (d) cha Sheria hii, Halmashauri inaweza kuteua Afisa kwa maandishi kwa ajili ya kukusanya ushuru na kodi hizo katika eneo husika. Aidha, kifungu cha 27 cha Sheria hii, kinazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa uwezo wa kuingia makubaliano na wazabuni au mawakala kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato katika vyanzo ambavyo vitakuwa vimebainishwa. Hivyo, utaratibu wa *Public Private Partnership* upo na unatumika katika Halmashauri kwa kuingia Mikataba na Wazabuni kwa ajili ya ukusanyaji wa ushuru huo. Kwa kutumia utaratibu wa Mawakala, Halmashauri zimebakiwa na jukumu la kusimamia na kudhibiti mfumo wa ukusanyaji wa ushuru ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Raya Ibrahim Khamis, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, mfumo wa ukaguzi na udhibiti upo na unatumika katika Halmashauri. Utaratibu unaotumiwa na Halmashauri kudhibiti mfumo wa ukusanyaji wa ushuru ni kuhakikisha kuwa vitabu vya risiti kwa ajili ya kukusanya ushuru, vinatolewa na Halmashauri husika kwa Mawakala au Watumishi wenyewe kadiri itakavyokuwa imeamuliwa na Halmashauri. Vitabu hivyo hukaguliwa kwa siku, kwa wiki au kwa mwezi na Afisa Mwandamizi aliyeulewa na Halmashauri na kukubaliwa na Baraza la Madiwani. Kadhalika kwa kwa wale wanaotumia Mawakala, Halmashauri hufanya ukaguzi wa kushtukiza katika maeneo ya makusanyo ili kujiridhisha kama vitabu vya risiti vinavyotumika ni vile vilivyotolewa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa mfumo huo wa udhibiti na ukaguzi, zipo changamoto za upotevu wa mapato kama vile baadhi ya mawakala kutumia vitabu vya risiti visivyokuwa vya Halmashauri na baadhi ya Halmashauri kutumia fedha kabla hazijapelekwa benki. Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kudhibiti hali hiyo zikiwemo kusimamishwa kazi, kupewa onyo na kufikishwa Mahakamani.

(b) Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, inaipa Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuingia mikataba na makampuni binafsi kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri. Hivyo, mfumo wa *Public Private Partnership (PPP)* ulishaanza kutumika katika Halmashauri zetu. Utumiaji wa *PPP* katika kukusanya ushuru umesaidia Halmashauri kupunguza gharama (*administrative costs*) katika ukusanyaji na kuongeza mapato.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Waziri, tatizo la upotevu wa mapato katika Halmashauri zetu limekuwa sugu. Pale mwanzo Serikali ilikuwa ikikusanya yenyewe na baadae ikazipa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya. Je, Serikali imegundua nini katika mifumo hii miwili; ule wa awali na wa sasa na hatimaye kupata dawa kwa ajili ya upotevu wa mapato katika Halmashauri zetu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, *I don't know* kama nimempata vizuri, lakini ninachokisema ni kweli anachosema kuwa, kuna wakati Halmashauri zenyewe zilikuwa zinaokota. Katika Bunge hili tumewahi kuitisha Sheria hapa ambayo imekwenda kufanya *pilot study* Dar es Salaam ili kuona namna ambayo tunaweza kuokota kitu kinachoitwa *Property Tax*.

Mheshimiwa Spika, *pilot study* ile sasa inamalizika ili tuone jinsi ambavyo tutakuwa tume-perform kule ili tuweze kuamua kama tuendelee na mfumo wa Halmashauri zenyewe ya kutoza au tuipeleke kwa hawa ambao tunawapelekea ambao tunawaita *private*, ambao wanafanya hivyo. Kwa hiyo, hii itakuwa imetusaidia. Pia ninataka kusema kuwa, baada ya kutumia hawa tumekuwa na changamoto nydingi; kuna sehemu unakwenda unakuta tukiokota wenyewe kama Halmashauri tunapata; wakati mwingine tunapookota kama Halmashauri kiasi kinachopatikana ni kidogo sana, unakuta gharama za kuzalisha nazo zinakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kuna *studies* mbalimbali zinazoendelea na Mheshimiwa Mchungaji Natse *has a point*; tutaona sasa ni mfumo upi ambao unafaa lakini sisi tuna- *operate* kwenye zile Sheria ambazo nimezielezea hapa.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa inaonekana kuwa huu mfumo wa *PPP* unachangia Serikali kupata mapato kidogo katika baadhi ya maeneo mengi ya nchi yetu. Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati mwafaka pengine iachane na utaratibu huu ikusanye zenyewe moja kwa moja na pesa zote ziweze kuingia Serikalini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, cha kwanza kabisa, nani anayeamua kuwa atumie utaratibu upi ni Halmashauri zenyewe husika. Ukiangalia hapa ninapata tabu kwa maana yule mwuliza swali wa mwanzo yeye huku chini anakuja kukwambia kuwa mnaona kama mngeachana na Halmashauri kuokota mkapeleka kwa hawa *private* kwa maana ya *Public Private Partnership*. Hii habari ya *ku-outsource is a modern way of living*, ndivyo ambavyo watu wanaishi sasa hivi, lakini ninasema kuwa kama tunafika mahali na sisi Bunge tunaona kuwa njia hii haitufai, basi ni kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa Halmashauri zenyewe ndiyo inayoamua itumie utaratibu upi; lakini kama Halmashauri ikiona ikitumia Halamashauri inaweza kuokota vizuri zaidi, hakuna haja ya kuendelea na mtu pale anachukua hela zenu. Tuna matatizo na kuna kesi nydingi tunapeleka Mahakamani mtu ameokota hela halafu hatuletei hizo hela. Kwa hiyo, sisi tunaelewa kinachozungumzwa hapa ni suala la Halmashauri zenyewe iamue.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa suala hili la ushuru limekuwa ni kero kwa baadhi ya maeneo kwenye Halamashauri zetu, kwa mfano; magari ya abiria yanayosafiri mwendo mrefu yanalazimishwa kuingia kila stendi hata kama gari limejaa na hakuna abiria anayeshuka ilimradi tu waende kutoa ushuru. Je, Serikali haioni sasa kuna sababu ya kutangaza kama kuna gari ambalo limejaza na halishushi abiria hakuna ulazima wa kuingia kwenye stendi hizo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, sijajua sasa uhusiano wa basi kujaa na kuingia na nini, kwa sababu kule tunapowaambia waingie, wanaingia kwa sababu tunatoza ushuru pale. Wakipita pale kwako Njombe wanatozwa wanalipa wanamaliza wanaondoka.

SPIKA: Wewe mwulize huko huko kwake, Njombe kunahusiana nini!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, mimi nimetoa mfano tu, *okay*, kwa hiyo, huko ambako kunasemwa.

Ninachotaka kusema hapa baadaye nitamwona Mbunge ili anielimishe vizuri anataka kusema nini pale. Tunachosema ni kwamba, amefika Same anaelekea Korogwe, akifika pale Halmashauri imeweka utaratibu kwamba basi likipita hapa litatozwa shilingi elfu mbili, *let say*, linapita pale linatoa halafu linakwenda. *Otherwise*, sasa Halmashauri itakachofanya ni kukimbizana na yale mabasi kuyafuata nyuma kumwambia wewe hukulipa na nini. Hilo ndilo ambalo mimi naliona.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, nitaomba nikae nae anielimishe vizuri.

Mheshimiwa Spika, usisahau kwamba, hapa pia kumekuwa na malalamiko kwamba, Halmashauri hazitozi ushuru wa kutosha na kwa matokeo hayo ni kwamba, sisi tunategemea zaidi ruzuku ya Serikali kuliko huu ushuru tunaozungumza hapa. Haya yote ni lazima tuyachukue sasa tuyaa galie kama tunaondoa hivyo na nini.

Nitakuomba Mheshimiwa Chilolo, tukae wote kwa pamoja unielimishe vizuri huo uhusiano wa kwamba kwa nini wanapitishwa kama gari halikujaa na vitu vingine vya namna hiyo.

Na. 3

Mradi wa Samaki wa Mapambo

MHE. DESDERIUS J. MIPATA (K.n.y. MHE. ABIA M. NYABAKARI) aliuliza:-

Katika Mkao wa Rukwa kuna Samaki wa Mapambo mbalimbali wanaovuliwa na Watalii kwenye Ziwa Tanganyika:-

(a) Je, tangu Watalii hao waanze kuvua samaki katika Ziwa hilo wameshavua tani ngapi?

(b) Je, Wananchi wa Mkao wa Rukwa wamenufaikaje na Mradi huo na kiasi gani cha fedha kimeachwa Mkoani Rukwa?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvubi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kulingana na Sheria ya Uvubi Na. 22 ya Mwaka 2003 na Kanuni zake za Mwaka 2009, kuna aina mbili za uvubi hapa nchini, ambazo ni uvubi wa samaki wa kawaida na uvubi wa burudani (*Sport Fishing*). Uvubi wa burudani hufanywa na Watalii kwa ajili ya burudani na siyo kwa ajili ya biashara. Uvubi wa samaki wa mapambo katika Ziwa Tanganyika hufanywa na wafanyabiashara wa samaki na samaki huvuliwa kwa kuzingatia taratibu za kawaida za uvubi na siyo Mradi kama ilivyoulizwa kwenye swali la msingi.

Mheshimiwa Spika, samaki wa mapambo huhesabiwa kwa idadi na siyo kwa uzito kama ilivyo kwa samaki wengine ambao huvuliwa kwa ajili ya chakula, kwa sababu samaki hawa

husafirishwa wakiwa hai. Kwa mfano, kati ya mwaka 2009 na 2012, samaki wa mapambo wapatao 223,000 walivuliwa katika Ziwa Tanganyika peke yake. Kuna aina nyingi za samaki wa mapambo katika Ziwa Tanganyika ambao baadhi yao ni pamoja na *Trophues*, *Petrochromis*, *Simochromis*, *Lamprologus*, *Neolamprologus*, *Xenotilapia*, *Tanganicodus*, *Julidochromis*, *Paracyprichromis*, *Spathodus*, *Altolamprologus*, *Variabilichromis* na *Cyphotilapia frontosa*.

(b) Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wamenufaika kutokana na uvuvi wa samaki wa mapambo katika Ziwa Tanganyika kwa kupata ajira, kwa sababu wafanyabiashara wanaovua samaki hao huwatumia wavuvi wa maeneo husika kwa ajili ya kuvua samaki hao na kuwahudumia hadi wanapofikia hatua ya kusafirishwa. Yapo makampuni matano yaliyosajiliwa yanayovua samaki wa mapambo ambayo yameajiri jumla ya wavuvi 44. Makampuni hayo ni *Tanganyika Sunshine* (14), *Nunu Mwamba* (9), *Tanzania Cichlids* (8), *NYAVITA* (6) na *Rift Valley* (7). Vilevile, makampuni husika hulipa ada ya leseni ya kukusanya samaki hao ambayo ni shilingi 20,000 kwa mwaka na ushuru wa kusafirishia samaki kutoka Ziwa Tanganyika kwenda Dar es Salaam kwa kiwango cha shilingi 40,000 hadi 60,000 kwa safari moja ya gari kulingana na kiwango kilichowekwa na Halmashauri husika. Aidha, makampuni haya hulipa ada ya leseni ya kusafirisha samaki wa mapambo nje ya nchi na ushuru wa kusafirisha samaki wa mapambo nje ya nchi. Fedha zitokanazo na ada na ushuru huo huingia Hazina na sehemu ya fedha hizi huingia katika Mipango ya Maendeleo ya Mikoa Nchini ikiwemo Mkoa wa Rukwa kuititia fedha zinazotolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kijiji cha Muzi, Kata ya Kasanga, wamenufaika kutokana na Kampuni ya Nunu Mwamba ambayo imetoa mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Wizara yangu inashauri makampuni mengine kujenga utamaduni kama huo wa kuwa na makubaliano ya namna hii na jamii iliyopo katika maeneo hayo iweze kujenga mahusiano mazuri na kufaidika na mikataba hiyo.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Wananchi wanaoishi Mwambao wa Ziwa Tanganyika ni maskini sana licha ya kuwa wamezungukwa na rasilimali nyingi. Mpango wa KILIMO KWANZA umekuwa mfano wa kuwakomboa wananchi wa namna hiyo. Je, Wizara ina mpango gani wa kuwawezesha Wananchi hawa wanaoishi katika Mwambao wa Ziwa Tanganyika wajkwamue kwa kufuata Kanuni ya KILIMO KWANZA kuwakopesha na kuwasaidia vitendea kazi?

(ii) Halmashauri ya Wilaya ya Nkansi pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga zimeathiriwa sana na utoroshwaji mkubwa wa samaki na dagaa na kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri hizo wameshindwa kabisa kudhibiti mapato kwa sababu samaki wabichi wanaovuliwa husafirishwa moja kwa moja kwenda Zambia. Je, Serikali ina mpango gani kuzinusuru Halmashauri hizi?

SPIKA: Samaki wa mapambo na wengine wabichi wa kula, Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, hili la kwamba, Wananchi wa Mwambao watanufaika vipi na KILIMO KWANZA, nataka kuamini kwamba, katika fikra hiyo tunazungumzia Wananchi wale katika hali ya uvuvi na namna watakavyonufaika na kazi yao ya uvuvi, lakini na shughuli zingine ambazo sasa zinaingia kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, Serikali imetengeneza mikakati ambayo inashirikisha Wananchi wenye na Halmashauri zenyewe ili tupate kunufaika na uwezo mkubwa wa uzalishaji hasa wa mazao ya chakula ambayo Mkoa wa Rukwa umedhihirika kuwa

ni katika mikoa yetu mikubwa inayozalisha chakula Tanzania. Kwa hiyo, mipango ya KILIMO KWANZA ipo na KILIMO KWANZA ni nadharia, mipango yenewe inakuja kwenye utekelezaji wetu sisi wenyewe na namna ambavyo tumejipanga katika ngazi ya Halmashauri mpaka ngazi ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, hii ya kwamba Halmashauri ya Sumbawanga na Halmashauri ya Nkasi inapoteza samaki wengi kutokana na kusafirisha samaki wabichi kwenda Zambia, hili ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kutokea Bandari ya Kipili kwa Mheshimiwa Ally Keissy na kutokea Bandari ya Kasanga huku chini, ni dhahiri kwamba hata mimi nilipokwenda kama Naibu Waziri wa Nishati na Madini, nimekuta hali hii ya kwamba bidhaa zinatoka kule; lakini ni kwa sababu naamini kwamba Wazambia walikuwa wamejitengenezea fursa nzuri zaidi ya kuwa na masoko makubwa zaidi ya samaki.

Mheshimiwa Spika, tumehimiza Watanzania hasa kwa sababu umeme unakwenda Kasanga sasa tunaweza na sisi kupata samaki wabichi, kuwatunza, kuwashimili na kusafirisha kwa ajili ya masoko.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, Serikali imejipanga kwa kuhakikisha kwamba Wananchi wa Sumbawanga na Nkasi wanapata manufaa zaidi kutokana na biashara hii ya samaki. Mipango mikubwa inategemea pia ianzie kwenye Halmashauri yenewe ambayo Mbunge pia ni mdau.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na samaki wa mapambo kuiingizia pato dogo sana nchi yetu, Tanzania inapoteza wastani wa dola milioni mia mbili na ishirini kila mwaka kutokana na mazao ya samaki hasa kwa Bahari Kuu. Serikali hadi leo haijajipanga hata kidogo kukusanya mapato haya. Je, Serikali ina mkakati gani na mpango gani hasa baada ya kuanzisha Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu kuhakikisha mazao haya ya Bahari Kuu yanapatikana ili Pato la Taifa lipatikane na Wananchi wa Tanzania waweze kufaidika na rasilimali hii?

SPIKA: Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwa ufupi mimi nadhani *figure* ya hesabu aliyotoa Mheshimiwa Hamad Rashid, inaweza ikawa sahihi kwamba tunapoteza idadi hii ya samaki. Upotevu huu wa samaki unatokana na uvuvi unaofanyika *Deep Sea* kule mbali ambako sisi hatujatengeneza uwezo wa kujilinda na maharamia wanaokuja kuiba samaki au kuvua samaki kwenye Bahari Kuu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa lakini tayari Serikali imejipanga hasa kutokana na matukio mbalimbali ambayo yamejitokeza na ninaamini kwamba, dawa ipo kwenye kutengeneza mikakati ya kuwa na uwezo wa kwenda Bahari Kuu kupambana na maharamia huko ili kuzuia wizi huo na Serikali inalifahamu hilo na inalifanya kazi.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, naomba kumwuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Anasema samaki Bahari Kuu wanaibiwa kwa sababu Serikali haijajipanga. Je, ni kwa nini Serikali imetoa leseni za kuvua katika Bahari Kuu ilhali wakijua hawana uwezo wa kufuatilia? (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Christina, jibu Mheshimiwa Waziri unataka kumwachia nani? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, tunatoa leseni kwa ajili ya uvuvi katika Bahari Kuu, lakini siyo kila uvuvi unaofanywa katika Bahari Kuu unapelekea kwenye wizi.

Mheshimiwa Spika, tunachosema ni hivi; tunapata manufaa hayo kidogo kutokana na uvuvi unaofanywa katika Bahari Kuu lakini tungeweza kupata manufaa zaidi kama kungekuwa na *defense mechanism* kubwa zaidi. Kwa hiyo, ndio maana tunasema kwamba, Serikali inataka kuwekeza ili tuwe na uwezo mkubwa zaidi wa kujilinda na hali hiyo, lakini hiyo haitazuia kwamba kwa nini tusitoe leseni.

Na. 4

Utaratibu wa Kukagua Bidhaa Nje ya Nchi

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Serikali imepitisha Sheria ya Ukaguzi wa Bidhaa Nje ya Nchi kabla haijasafirishwa kuletwa nchini kwa lengo la kudhibiti bidhaa zisizo na viwango:-

- (a) Je, mafanikio gani yamepatikana tangu kuanza kwa utaratibu huo?
- (b) Je, utaratibu huu unafanyika katika nchi gani?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Ukaguzi wa Bidhaa Nje ya Nchi (*Pre-shipment Verification of Conformity to Standard - PVOC*) ya Mwaka 2009, iliyoanza kutumika rasmi mwezi Februari, 2012, kwa lengo la kudhibiti bidhaa zisizo na viwango nchini. Mafanikio kadhaa yamepatikana kama ifuatavyo:-

- (i) Kupungua kwa kiasi kikubwa msongamano wa mizigo inayohitaji kukaguliwa ubora wake katika Bandari ya Dar es Salaam;
- (ii) Kupungua kwa bidhaa zenye ubora hafifu kwenye masoko yetu na hivyo kuepusha soko letu kuwa dampo la bidhaa zisizo na ubora na kuharibu mazingira;
- (iii) Kuondoa ushindani usiokuwa na haki utokanao na uuzwaji wa bidhaa zenye ubora hafifu kutoka nje na hivyo kulinda viwanda vya ndani;
- (iv) Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*) kuititia wakala wake, kupata fursa ya kufanya ukaguzi wa bidhaa zote nje ya nchi bila kujali matabaka ya bidhaa zenyewe (*Red, Green na Yellow Channels*); na

(v) Kuongezeka kwa bidhaa zinazoingia kwa kupewa vyeti vya ubora. Mfano, hadi kufikia Novemba, 2012, kiasi cha mizigo 16,946 iliweza kupewa vyeti vya ubora, ambapo hapo mwanzo hapakuwa na takwimu rasmi za bidhaa zinazoingia.

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa ukaguzi wa bidhaa kabla ya kusafirishwa hutekelezwa katika nchi zipatazo 188 duniani kote. Aidha, nchi jirani za Kenya, Uganda, Ethiopia, Zambia na Nigeria ni mionganoni mwa nchi zinazotumia mfumo huu na zimefanikiwa sana.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Lengo na madhumuni ya utaratibu huu ilikuwa ni pamoja na kuepusha hasara itokanayo na bidhaa kuharibiwa hapa nchini zinapobainika hazina viwango na pia kuondoa bidhaa zisizo na ubora kabisa. Hivi karibuni Waziri wa Biashara na Viwanda, alikaririwa akisema ongezeko la bidhaa feki katika nchi yetu limefikia asilimia 30. Jibu liliopo hapa linasema kwamba, tumepata faida ya kupungua kwa ongezeko la bidhaa zisizo na ubora: Je, ni takwimu gani sahihi zinazoonesha tumepata ahueni ya kuingia kwa bidhaa zisizo na ubora katika nchi yetu? Tunaomba jibu kwa takwimu.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu, anaweza kukosa takwimu lakini atakujibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ni kweli lengo kuu ni kudhibiti bidhaa hizi na kama Mbunge alivyosema kwamba, Waziri alitamka kuwa ongezeko sasa hivi ni asilimia 20 mpaka 30 ya bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba nillieleze Bunge lako Tukufu kwamba, tatizo kubwa si Sheria yenyewe, tatizo kubwa ni utekelezaji wake. Maana ya utekelezaji ni kwamba, wale wakala ambao wanadhibiti hizi bidhaa nje ya nchi ndiyo wenyewe matatizo kwa kukosa uaminifu, siyo waadilifu, wanatuungiza katika hali mbaya sana mawakala. Sheria yenyewe haina matatizo. Vile vile uhaba wa watumishi ambao tunao katika *TBS* nao unachangia kwa kiasi kikubwa katika udhibiti wa mambo haya hasa kule kwenye mipaka yetu.

Vile vile wafanyabiashara wenyewe ambao kwa kweli nao wamekosa uadilifu, wamekosa uzalendo na wanafanya mambo ambayo ni kinyume kwa kupitisha bidhaa njia za panya.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi *TBS* inajaribu kufanya tathmini juu ya utendaji kazi wa mfumo huu na wanatarajia kutoa taarifa hii ifikapo mwezi Machi mwaka huu wa 2013 na kama itabainika kwamba, ipo haja basi Sheria hii inaweza ikaletwa hapa kwa maana ya kuboresha Sheria iliyopo na Wabunge mtapata fursa ya kuweza kuchangia vizuri.

MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa bidhaa hizo zinakaguliwa nje ya nchi na kuingia nchini zikiwa na *certificate*.

Je, Serikali inatumia njia gani za ziada kujihakikishia kuwa bidhaa hizo zina ubora mbali na *certificate* ambazo zinakuja na bidhaa hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri umemwelewa; yaani ziada unatumia nini sasa! Naomba ujibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, mbali na kutoa *certificate* ni kwamba, unafanya ukaguzi kuitia katika maeneo mbalimbali yakiwemo maduka ambako bidhaa hizi zinapika na huwa inakaguliwa na *TBS* kuangalia kama vifaa au bidhaa ambazo zimeingia kwenye maduka hayo au sehemu mbalimbali zinakidhi au hazikidhi, na kama hazikidhi, sasa hivi tunayo sheria ya kuteketeza au kuchoma hizo bidhaa ambazo hazikidhi.

SPIKA: Swali linalofuata, Mheshimiwa Missanga. Endelea.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, kabla sijauliza swali langu, nieleze tu masikitiko yangu kwamba maelezo ya msingi ya swali hili hayakuwekwa. Kwa hiyo, sina hakika kama wapiga kura na wananchi wataelewa swali langu. Lakini kwa maelekezo yako umesema niendelee, naomba basi swali langu namba tano, sasa ijibewe.

Na. 5

Hitaji la Viwanda Mikoani

MHE. MOHAMED H. MISSANGA aliuliza:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kutojenga viwanda Mikoani kunasababisha vijana wengi kukimbia Dar es Salaam jambo ambalo linaweza kusababisha vurugu na uvunjifu wa amani nchini?

(b) Je, Serikali haioni ni vyema na busara kutawanya viwanda Mikoa mbalimbali ili kuweka usawa wa bei za bidhaa muhimu kama vile mabati, sementi, nondo na kadhalika ambazo hivi sasa zinazwa bei ghali Mikoani ikilinganishwa na Dar es Salaam kuliko ilivyo hivi sasa?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutokuwepo na viwanda vya kutosha Mikoani ni sababu mojawapo ya vijana wengi kukimbia Mijini hususan Dar es Salaam ambako pia kuna fursa na vivutio vingi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, suala la ujenzi wa viwanda kwa sasa linatekelezwa na sekta binafsi ama kwa utaratibu wa *Public Private Partnership - PPP*. Aidha, jukumu la Serikali kwa kiasi kikubwa limekuwa ni kuandaa sera nzuri na kuweka mazingira wezeshi yatakayoiwezesha sekta binafsi kutekeleza jukumu la kujenga viwanda. Hata hivyo, Serikali kuitia Mamlaka ya maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje (*EPZA*), imeweza kutenga maeneo katika Mikoa yote nchini ikiwemo Mkoa wa Singida isipokuwa kwa Mikoa mipyä ili kutoa fursa kwa wawekezaji watakaojitokeza katika Sekta ya Viwanda kufanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, suala la kutawanya viwanda katika Mikoa mbalimbali hapa nchini ikiwemo Mkoa wa Singida ndiyo nia ya Serikali. Hata hivyo, kwa sehemu kubwa, ujenzi wa viwanda vyenyewe ni utashi wa mwekezaji kulingana na fursa anazoziona kama vile malighafi ya kutosha kwa ajili ya kiwanda chake, huduma muhimu kama zinapatikana ikiwemo (maji, umeme, mawasiliano, barabara na kadhalika) na soko la bidhaa atakayozalisha.

Mheshimiwa Spika, jukumu la Serikali bado litaendelea kuwa, kutenga maeneo na kuweka miundombinu itakayowavutia wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika maeneo mbalimbali Mikoani na nchini kote.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo aliyoeleza, lakini kwa upande wa pili, majibu haya hayaridhishi kwa sababu yanadahirisha ile nia niliyosema kwamba Serikali haina mpango wa kuendeleza Mikoa mbalimbali kwa viwanda na kuendelea kujenga viwanda Dar es Salaam pekee yake. Hakuna mpango!

Kwa hiyo, mawazo haya kama mtazamo ni Dar es Salaam tu, jambo ambalo nimelisema ni hatari. Kwa mfano, katika jibu lake la pili amesema, kama Mikoa wa Singida una maji ya kutosha, una umeme, una mawasiliano, una barabara, una soko la uhakika na malighafi, Singida pale Manyoni kuna *gypsum*, kuna uwezekano kabisa wa kujenga kiwanda cha sementi na hakuna sementi kabisa katika hii *central corridor*.

Singida vile vile kuna mafuta ya alizeti, tungeweza kabisa kujengewa kiwanda kikubwa cha alizeti cha kufanya *double refinery*. Singida kuna dhahabu ingewezekana kabisa kuweka kiwanda pale cha kusafisha dhahabu; Singida kuna asali nzuri kuliko asali zote hapa Tanzania, ingewezekana kabisa kuweka kiwanda pale:-

(a) Je, kwa sababu tunakidhi jibu namba mbili ambalo Mheshimiwa Waziri amesema, bado Serikali haioni kwamba ni kazi yake kushawishi huyo mwekezaji *under PPP?* Ni kazi ya Serikali kushawishi kuangalia maeneo yake kuondoa hii kasumba ya watoto kutoka Vijijini kuja Dar es Salaam? Hilo swalii la kwanza. (*Makof!*)

(b) Lakini swalii la pili, basi kama haiwezekani kuweka viwanda pale Singida, Singida ndio katikati ya Tanzania. Barabara sasa ni safi, reli ipo: Kwa nini Serikali isiweke hapo pale Singida ili mizigo yote inayotoka Bandari ya Dar es Salaam na nyinginezo ije pale Singida, wenzetu wa Burundi, Rwanda, Congo, Uganda na wengine hawa wote waje wachukulie pale, jambo ambalo litaondoa *congestion* katika barabara yetu hii ya kuja Dar es Salaam?

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunazungumza, ndio mwelekeo wa Sera ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo yako *potential* au yana rasilimali ambapo tunaweza tukayaendeleza tunalenga huko. Mathalan, tunapozungumza Mikoa wa Singida; dakika hii tunazungumza, tunawekeza umeme pale wa *Megawatt* kuanzia 50 mpaka 300 kwa utaratibu wa *PPP* na tutagharamia dola milioni 136 na mradi huu tunaushughulikia dakika hii ili kuanzia pale Singida tuweze tukawa na chanzo cha umeme ambacho kitasaidia kwa ajili ya msukumo wa uzalishaji katika eneo hilo.

Vile vile uzalishaji katika Mikoa wa Singida wanazalisha vizuri zao la alizeti kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza. Serikali tunatazama namna ya kuwawezesha zaidi wananchi wa maeneo hayo ili kilimo hicho na uwekezaji katika *Agro processing* uweze ukakidhi mahitaji ya uzalishaji wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kiujumla Serikali ina mwelekeo wa kutazama namna ya kusaidia na kuzalisha maeneo ambayo rasilimali ipo pale. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Fedha kwa sababu huyu anasema tulimnyima maelezo, kwa hiyo, nimemwachia aeleze. Kwa hiyo, naomba tuendelee. Mheshimiwa Mangungu kwa niaba ya Mheshimiwa Mkapa uliza swalii linalofuata.

Tawi la NMB Mangaka Kufanya Kazi kwa Siku Sita

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. DUNSTAN D. MKAPA) aliuliza:-

Je, ni lini Tawi la *NMB* Mangaka Wilayani Nanyumbu litatoa huduma kwa siku sita kwa wiki kama ilivyo kwa Matawi mengine nchini?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki ya *NMB* Tawi la Nanyumbu lililopo Mangaka (*NMB* Nanyumbu) lilianza kufanya kazi tarehe 21/9/2011. Tawi hili lilianza kama tawi dogo kwa kutoa huduma kwa wananchi wakati ambapo huduma zilikuwa zinatolewa mara tatu kwa wiki katika siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa wakati Benki ikiwa inaangalia ukuaji wa kibiashara katika eneo ille. Baada ya kuimarika kwa shughuli za kibiashara katika eneo husika, Benki ilianzisha utaratibu wa kutoa huduma kwa siku sita kama matawi mengine yote ya *NMB*. Utaratibu huu uliana tarehe 25 Oktoba, 2012. Aidha, tathmini iliyofanyika inaonekana kwamba kwa sasa hali ya utendaji ni ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya matawi mapya yanayotarajiwa kufunguliwa mwaka huu kati ya Februari mpaka Aprili kwa Mkoa wa Dar es Salaam ni Tawi la Uwanja wa Ndege (kwa ajili ya huduma za uhamiaji), Kariakoo, Ubungo Plaza, Mwanakwerekwe kule Zanzibar, Tabata (barabara ya Nelson Mandela), Sinza, Buguruni, Mbezi (*Morogoro Road*) na Tandika.

Matawi mengine ambayo yatafunguliwa Mikoani ni pamoja na Buzurugwa (Mwanza), Himo (Kilimanjaro), Kaliua (Tabora), Kishapu (Shinyanga), Iringa, Dodoma, Kakonko (Kigoma), pamoja na Wilaya tano ambazo ni mpya. Sambamba na ufunguzi huu, matawi ya Bariadi, Geita, Mpanda na Njombe yatapandishwa hadhi na kuwa matawi ya Mkoa.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini naamini kabisa hata ye ye mwenyewe majibu aliyyoyatao hayawiani sana na swalii ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Mkapa. Tunachotaka kujua utaratibu wa kuweka *agency* katika kila maeneo ulikuwa ukifanyika tangu ilipokuwa *NBC*.

Tunataka kujua kwa nini pamoja na biashara kukua katika Tawi hili ambalo limetamkwa la Mangaka, haliwi katika *operations* za kawaida kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi? Sababu zipi ambazo zinatuzuia? Swalii la kwanza.

La pili, yapo maeneo ambayo yanakua sana kiuchumi na kunakuwa na shughuli nydingi sana ikiwemo Somanga, Nangulukuru, Kipatimo: Kwa nini sasa Serikali kuititia *BoT* wameweka masharti ya ubebaji wa pesa lazima iwe inabebwa na magari maalum? Kwa Miko ya Lindi na Mtwara magari haya yanapatikana Mtwara pekee yake.

Je, gari litawezza kutoka Mtwara kwenda mpaka Kilwa lubebe pesa kupeleka Somanga; hatutumii Polisi ambaao wameajiriwa na Serikali hii na wamekula Kiapo cha Utii kuitumikia nchi hii wakalipwa posho na wakapewa uvezeshaji mwingine kama wanavyopewa Makampuni binafsi

na Polisi wanakaa hawalipwi posho? Sheria hii itatenguliwa lini ili sisi wananchi wetu wasiendelee kupata shida?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Lakini swali la kwanza alijibu, wewe tu hukusikia.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza nimemwambia kwamba sasa hivi toka kuanzia tarehe 25 Oktoba, 2012 Tawi hili linafanya kazi kama yalivyo matawi mengine ya *NMB*. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia kwamba Tawi hili linaendelea kufanya kazi. Pale mwanzo tulikuwa tunaangalia inakuaje na ndipo tulipoona biashara ni ya kuridhisha, basi tumeweza ku-*employ* na sasa hivi kuanzia tarehe 25 Oktoba, 2012 Tawi hili linafanya kazi zake kama kawaida.

Kuhusu suala la sehemu nyingine ambazo alizitaja Mheshimiwa Mbunge, kwanza uamuzi wa kuweka matawi katika sehemu husika haitokani tu na kuridhishwa kwa biashara inayokuwa inaendelea pale kwa sababu kuweka Tawi pale ni *expenses* na *NMB* lazima iwe na mipango madhubuti kuona kwamba biashara zile zinakuwa *operational*.

Kuna mipango ya kazi (*human resource planning*) ya watendakazi, ni uamuzi wa *reallocation* ama tunaweza tukapata *recruitment* ama tunaweza tukafanya *deployment*, mtu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine. Lakini vile vile kuweka tawi kunahitaji vile vile *financial planning*.

Watu pale wanahitaji kulipwa, watu wanahitaji ulinzi na majengo. Vile vile na hii imekuwa ni tatizo kubwa hususan kupata majengo ya kuweka Tawi. Lakini *economic aspect* nayo inaingia kati. Unaweza ukaweka Tawi, lakini ikawa *return* ambazo umeziweka pale haziridhishi.

Kwa hiyo, inakuwa tunakwenda kwa hasara zaidi kuliko faida inayopatikana. Katika sehemu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, naomba tu nikutane naye ili tuweze kuangalia huo uwezekano kama yeye alivyokuwa ametaja kwamba kuna *potential* maeneo yale ambayo ameyataja ili tuangalie *plan* yetu inayokuja tunaweza kuli-*take* vipi suala hili. Ahsante.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 12 tu ya Watanzania wanaotumia mitandao rasmi ya Kiserikali ya fedha, yaani *NMB* na Benki kama hizo, lakini zaidi ya asilimia 50 ya Watanzania wanakwenda kwenye mitandao mingine isiyo rasmi kama vile *Vodacom*, *Tigo* na kadhalika. Je, Serikali inasema nini? Inajifunza nini juu ya hii *shift* ya Watanzania kutotumia Benki zao na badala yake wanatumia mitandao ambayo siyo rasmi? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MUKYA SALUM): Mheshimiwa Spika, kweli nakubaliana naye kwamba asilimia 12 tu ya Watanzania ndio ambao wanatumia *banking services* kwa kutumia benki, lakini asilimia 50 alivyoisema yeye kwamba wanatumia hii *services* ambayo haiko rasmi, kwanza napenda kumhakikishia kwamba M-Pesa, Z- Pesa, Tigo - Pesa yote ni mitandao rasmi na imesajiliwa kufanya kazi kama kutoa huduma hizi za kibenki. Kwa hiyo, nayo inakua

Serikali tayari ina-*recognize* huduma ambazo zinatolewa na mitandao ya simu kwa huduma za *banking services*. Mwaka 2012 tayari tumerekebisha angalau *regulations* za kuweza kuona ni jinsi gani sasa tutaweka mazingira mazuri kwa ajili ya asilimia hii 50 ya Watanzania

kuweza sasa ku-*recognize* kwamba wanatumia hii mitandao ambayo inatoa huduma za simu, lakini vile vile inatoa *banking services*. Lakini napenda vile vile kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, labda nimkumbushe kwamba, kama nilivyokuwa nimesema, kuamua tu kwenda kuweka Benki ama Tawi ni gharama kubwa sana, inategemea sana *returns* zile ambazo zinapatikana pale.

Kwa hiyo, naomba Benki nyingi sasa hivi, kwa sababu Benki ni biashara, wanaangalia jinsi uwezekano wa wao kupata biashara sehemu ambazo zinahusika na Benki nyingine zina *strategic plan* kwa mfano *Federal Bank of Middle East* tayari katika *strategic plan* yao wao wanataka ku-*operationalise* sehemu chache sana kwa ajili ya kuweza ku-*Maintain customers* wao.

Kwa hiyo, inategemea sana zile Benki kwenye *strategic plan* zao hasa wao wenyewe wanataka nini?

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba 50% wanaotumia huduma za simu kama ni *banking services*, tayari zinakuwa *recognized* na Serikali.

Na. 7

Wananchi wa Rarya Kufaidika na Maji ya Ziwa Victoria

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE (K.n.y. MHE. LAMECK O. AIRO) aliuliza:-

Ziwa Victoria ni miuongoni mwa maziwa makubwa duniani na Wilaya ya Rarya imebahatika kumiliki sehemu kubwa ya Ziwa hilo, lakini wananchi wake wanataabika sana na shida ya maji:-

Je, ni lini wananchi wa Rarya watanufaika na maji ya Ziwa Victoria?

(a) Je, Serikali ina mikakati gani mahsus i ya kulinda mazingira ya Ziwa hilo?

WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lameck Okumbo Airo, Mbunge wa Rarya, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, wananchi wa Wilaya ya Rarya wameanza kunufaika na maji ya Ziwa Victoria. Kati ya mwaka 1970 na 1975, Serikali ilijenga miradi minne inayotumia maji ya Ziwa Victoria iliyolenga kuhudumia Vijiji 13. Vijiji hivyo ni pamoja na:-

(i) Mradi wa Maji Shirati unaohudumia Vijiji sita vya Mkoma, Kyariko, Raranya, Nyahera, Masonga (kitongoji kimoja), na Nyamagongo (kitongoji kimoja);

(ii) Mradi wa Maji Komuge unaohudumia Vijiji sita vya Kyamwani, Komuge, Kuruya, Irienyi, Baraki, (kitongoji kimoja) na Bitiryo;

(iii) Mradi wa Maji wa Kyangasaga unaohudumia Kijiji cha Kyangasaga;

(iv) Mradi wa Maji wa Masonga/Nyamagongo unaohudumia Vijiji vya Masonga na Nyamagongo. Miradi hiyo ni ya muda mrefu na itaendelea kufanyiwa ukarabati na Serikali ili kuboresha ufanisi wa utoaji wa huduma ya upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, kuititia Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji, Serikali itajenga miradi minne itakayotumia maji ya Ziwa Victoria. Miradi hiyo ni ya Vijiji vya Kinesi, Kirogo, Baraki na Nyihara.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatekeleza mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, Ukanda wa Pwani, maziwa, mito na mabwawa makubwa tangu mwaka 2008 kuititia Mradi wa Hifadhi ya Mazingira wa Ziwa Victoria awamu ya pili. Mkakati huo unahusu kazi zifuatazo:-

(i) Kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kudhibiti magugu maji;

(ii) Ujenzi wa mfumo wa majitaka katika Miji ya Mwanza na Bukoba pamoja na ujenzi wa miundombinu katika maeneo oevu (*wetlands*) kwa ajili ya kusafisha majitaka ya viwandani na majumbani;

(iii) Kutoa elimu kwa jamii za wengine viwanda juu ya utunzaji wa vyanzo vya maji;

(iv) Kuhamasisha ujenzi na utumiaji wa vyoo vya jumuiya kwenye mialo katika kila Wilaya za mwambao wa Ziwa Victoria; na

(v) Kuwezesha wananchi kuibua na kutekeleza miradi midogo midogo ya jamii inayolenga kuhifadhi mazingira ya Ziwa Victoria.

MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ni kuhusu vikundi vya kijamii kuhusu kutunza na kuhifadhi mazingira. Viko vikundi vingi vya *BMUs* (*Beach Management Units*); Serikali ina mpango gani kuimarisha vikundi hivi ikiwa ni utaratibu endelevu?

Pili, Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali yetu shupavu chini ya Chama cha Mapinduzi, imeweza kutoa maji kutoka Ziwa Viktoria mpaka Kahama, zaidi ya kilomita 200. Lakini Serengeti ambako ni kilomita 200 tu kutoka Ziwa Viktoria ambako usambazaji wa maji ni kama 32% na ni sehemu ya kuvutia watalii na kuendeleza jamii; Serikali, ina mpango gani kutoa maji Ziwa Viktoria kwenda Wilaya ya Serengeti? (*Makofii*)

WAZIRI MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nakubaliana kwamba, kuna vikundi vingi vya jamii ambavyo, vinashiriki katika uhifadhi wa mazingira katika mwambao wa Ziwa Viktoria. Hivi sasa Serikali, ikishirikiana na wanachama wenzake wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, inatekeleza miradi midogomidogo ya uhifadhi wa mazingira katika Ziwa Viktoria, 126 na utekelezaji uko katika Wilaya ambazo ziko mwambao na zinapakana na Ziwa Viktoria na zile ambazo ziko katika Mikoa ya Uagenda wa Ziwa Viktoria.

Pili, Mheshimiwa Spika, Serikali, inasanifu miradi mbalimbali ya maji ya kutoka Ziwa Viktoria pamoja na kuangalia uwezekano wa kuchukua maji katika maeneo na vyanzo vingine katika eneo hilo. Ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuupatia maji Mji wa Serengeti, kutoka ardhini, kutoka katika mabwawa, kutoka katika mito iliyopo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, chanzo ambacho kitatumika kinalenga kupunguza bei, kinalenga ubora wa maji, kinalenga urefu ambao chanzo hicho kinawenza kutumika, ama miaka 10 au miaka 20. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba, Wizara yangu inaangalia kwa makini namna ya kuupatia Mji wa Serengeti, maji ya kutosha katika muda mfupi, ili kukidhi mahitaji ya maji katika mji huo.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wilaya ya Rarya, Wilaya Mama yake ni Wilaya ya Tarime na kwa kuwa, Wilaya ya Tarime iko umbali upatao kilomita 15 kutoka Ziwa Viktoria, naomba Kauli ya Serikali; iwaambie wananchi wa Tarime, ni lini watapata maji safi na salama kutoka Ziwa Viktoria?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Tarime iko kilomita 15 kutoka Ziwa Viktoria. Hivi sasa Tarime inatekeleza Mradi wa Maji Safi na Salama na Usafi wa Mazingira. Katika kutekeleza miradi hii, wananchi wakashirikiana na Mshauri wa Mradi pamoja na Wataalamu wa Wilaya ya Tarime, wamechagua vyanzo vya maji. Namkaribisha Mheshimiwa Nyangwine, aje Ofisini tuzungumze tuone ni jinsi gani utekelezaji wa Vijiji vya mbele zaidi au vinavyofuata vinawenza kufaidika na chanzo cha Ziwa Viktoria.

SPIKA: Na wengine wanataka kusikia, sasa mkikaa Ofisini wengine watasikiaje?

Na. 8

**Kufungwa kwa Kitengo cha Watoto
Wasioona – Mpanda Mnyaki**

MHE. RITA L. MLAKI (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR) aliuliza:-

Kitengo Maalum cha Wototo Wenye Ulemavu Wasioona Wilayani Mpanda Mnyaki, Shule ya Msingi Katumba, kimefungwa na hakuna Mwalimu hata mmoja mpaka sasa:-

Je, ni sababu gani zilizosababisha kufungwa kwa Kitengo hicho, huku kukiwa na walimu wengi wa taaluma, wanaosubiri kuajiriwa?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nieleze kuwa, hakuna Wilaya ya Mpanda Mnyaki, bali kuna Wilaya ya Mpanda; katika swali la msingi, liliulizwa hivyo. Pia, shule yenye Kitengo siyo Katumba bali ni shule ya Msingi Mnyaki, yenye jumla ya wanafunzi 1,408 na Walimu 19 akiwemo Mwalimu mmoja Mtaalam wa Elimu Maalum wa Fani ya Viziwi na sio fani ya wasioona, ambapo shule hii ipo katika Kata ya Nsimbo; Shule hii imejengwa katika eneo liliokuwa Makazi ya Wakimbizi toka Burundi.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Mnyaki, ina Kitengo cha Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum, kilichoanzishwa na Walimu watatu mwaka 2003, Wakimbizi wawili, raia wa Burundi na raia mmoja Mwalimu Mtanzania, waliopata mafunzo kutoka Chuo chetu cha Elimu, Patandi. Baada ya amani kupatikana nchini Burundi, Wakimbizi ikiwa ni pamoja na Walimu Wataalam wale wawili, walirejea kwao Burundi mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, Wakimbizi hao walipoondoka Kitengo cha Watoto Wenye Mahitaji Maalum cha Shule ya Msingi Mnyaki, kimebakni na Mwanafunzi mmoja tu mvulana na ni Mtanzania. Na anakilema cha ukiziwi, ambaye kwa sasa yupo darasa la sita; hivyo, Kitengo kipo hakijafungwa.

Mheshimiwa Spika, mwanafunzi huyu mwenye ulemavu amejumuishwa katika darasa la wanafunzi wasio na ulemavu (*Inclusive Education*) na kupatiwa kifaa kinaitwa *Audio Meter*, kinachomsaidia kusikia ili aweze kuendana na mafundisho. Aidha, Kitengo kitaendelea kuwaandikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, wakiwemo wasioona kadiri ya upatikanaji wa watoto hao kutoka kwenye mazingira yanayozunguka maeneo ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali, itaendelea kuajiri Walimu wenye ujuzi wa kufundisha watoto wenye mahitaji maalum kila mwaka, ili kukidhi mahitaji ya shule katika Halmashauri husika.

MHE. RITA L. MLAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri na ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa, kuna shule za namna hiyo za Walemvu na za kawaida ambazo ziko katika mazingira magumu na kuna Wafadhili kutoka Austria amba wamejenga kwa mfano, Shule ya Engaruka huko Momela. Je, Serikali, ina mpango gani wa kuwapelekea Walimu, Shule kama hizi ambazo zimejengwa na Wafadhili, kwa ajili ya kusaidia wanafunzi walioko katika mazingira magumu?

Pili, Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani kusamehe kodi kwa vifaa ambavyo vinachangwa na wananchi wa Austria, wanaoleta katika Shule hii ya Engaruka na vifaa hivyo vinaku bila kuwa na faida yoyote?

Mheshimiwa Spika, naomba jibu langu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza muuliza swali, Mheshimiwa Mbunge, lakini vilevile na Mheshimiwa Ritta Mlaki, kwa kuuliza maswali ya nyongeza. Hiyo shule anayoitaja ni kweli na mimi nilikwenda mwaka jana, nikakuta iko kwenye mazingira hayo magumu na nikawa nimewaahidi kwamba, tutakapokuwa tunapanga Walimu mwezi huu tutawapatia Walimu kadiri ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa kwamba, Walimu tumeshapanga tayari pale Wizarani na kwa Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge na tuliahidi kwamba, angalau mwezi Januari na Februari, Walimu tutakuwa tumeshawasambaza huko. Tumeshapata tayari kibali kutoka Utumishi, tunasubiri tu mifumo ya fedha ili Walimu hawa tutakapowapanga kwenye Halmashauri huko, tena wasihangaike kwamba, hawana fedha za kujikimu na hivyo wanaanza kuandamana. Lakini ni wakati wowote tutaanza kupeleka Walimu kwenye Halmashauri zote.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kusamehe kodi za vifaa vya kufundishia. Labda hapa nieleze kidogo kwamba, imekuwa ni desturi ya hizi *NGO*, zinafika pale Bandarini, wanatupigia simu kwamba, kuna vifaa vya kufundishia hapa na hata vifaa vya walemvu, lakini baadhi ya *NGO* unakuta hazijishughulishi na masuala haya ya elimu, labda hivyo vifaa wanakwenda tu kuuza. Kwa hiyo, kinachotakiwa hapo Waheshimiwa Wabunge, kwa faida ya wote na Mheshimiwa Ritta Mlaki, sisi Wizara ya Elimu, tupate barua inayosema kwamba, *NGO* itajishughulisha na masuala ya kugawa vifaa vya Walemvu au vya kufundishia, vitabu na kadhalika, lakini tuwe na uhakika kwamba, kweli mnafanya mambo hayo.

Mheshimiwa Spika, sisi tukisha-*approve* hilo, tutaandika barua pale Wizara ya Fedha, TRA, hivyo vifaa haviwezi kutozwa kodi kama ambavyo huwa havitozwi kodi kwenye shule na vyuo kama tunavyofanya kwenye Wizara ya Elimu. Ahsante sana.

Na. 9

**Barabara ya Kilimanjaro Machine
Tools – Machame Gate**

MHE. JOSEPH R. SELASINI (K.n.y. MHE. FREEMAN A. MBOWE) aliuliza:-

(a) Je, barabara ya *Kilimanjaro Machine Tools – Machame Gate* Wilayani Hai, ina kilometra ngapi na ilijengwa mwaka gani kwa kiwango cha lami?

(b) Je, barabara hiyo imefanyiwa *full resurfacing* mwaka gani?

(c) Je, Serikali, ina mpango gani wa kuikarabati barabara hii kwa kupanua, kuweka sehemu za watembea kwa miguu na mifumo ya maji?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara ya *Kilimanjaro Machine Tools – Machame Gate*, ina urefu wa kilomita 15 na ilijengwa kwa kiwango cha lami katika miaka ya 1951 na 1954.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara hiyo imekuwa ikifanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa awamu, hususan katika maeneo yaliyokuwa yamechakaa zaidi. Hadi sasa sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilomita saba, imeimarishwa kwa kuwekewa tabaka lingine la lami nzito (*Asphalt Concrete*) kati ya mwaka 2008 na mwaka 2012.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali itaanza kutenga fedha za kuipanua, kujenga sehemu ya watembea kwa miguu na kuimariswa mifereji ya maji katika barabara hii kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa, barabara hii imejengwa tangu mwaka 1951/1954 na ni takribani miaka 60 sasa na kwa kuwa, swalii la msingi, linauliza suala la maji ambayo ni adui mkubwa wa barabara (*Drainage System*), linauliza upanuzi wa barabara, linauliza *routine maintainance*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, hivi ni vigezo muhimu katika sekta ya Uhandisi Ujenzi. Tatizo kubwa kwenye barabara zote za milimani hasa za maeneo ya miinuko, Serikali inapotoa Mikataba kwa Wakandarasi kujenga barabara hizi, wanaishia kwenye *level* ya *monitoring and evaluation*. Je, *level* ya *risk management* na *routine classification*, ambazo hazitekelezwi ipasavyo kwenye barabara nyingi za nchi yetu, zinazosababisha mzunguko wa upotetu mwingu wa fedha za walipa kodi wa nchi hii na Kitengo hiki cha *Risk Management*, mpaka leo hii hakipo kwenye Wizara ya Ujenzi. Je, Serikali, inasema nini kuhusu kuokoa fedha za walipa kodi wa nchi hii kwenye ujenzi wa barabara hasa Kitengo cha *Risk Management*?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la Msingi kwamba, barabara hii ilijengwa miaka ya 50. Kwa hiyo, ina maana ule usanifu, muda wa

barabara kudumu katika muda unaotegemewa umepita na ndio maana tumesema tunaanza kuifanyia upanuzi. Sasa mnapofanya upanuzi ina maana haya masuala yote tunayozungumza ni lazima muyaweke kwenye mpango, muangalie ni namna gani mifereji itajengwa.

Mheshimiwa Spika, hayo masuala ya *Risk Management* si lazima tuwe na Kitengo, Wahandisi ambao tunao wanafahamu mambo yote haya ya *risk management*. Kwa hiyo, wanaweza kufanya katika usanifu na kusimamia matengenezo yake inavyotakiwa.

Na. 10

**Tanzania Building Agency Kuwajali
Wateja Wao**

MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI aliuliza:-

Siri ya mafanikio ya biashara yoyote ni pamoja na kuwajali wateja wake:-

(a) Je, ni kwa nini, *Tanzania Building Agency (TBA)* inakosa utu wa kuwajali wateja wao hata pale wanapoibiwa?

(b) Je, kwa nini, wahusika wa ulinzi walioajiriwa na *TBA* wakati wa tukio la wizi wa kufanana hawaguswi na hawaulizwi na viongozi husika wa karibu nao wanahusika vipi?

(c) Je, kwa nini *TBA* isivunjwe na kazi zake zikafanywa na *NHC*, Shirika linalojali wateja wake?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la msingi lenye vipengele (a), (b) na (c) la Mheshimiwa Dokta Maua Daftari, naomba nitoe maelezo ya ufanuzi kama ifuatavyo:-

Wakala wa Majengo (*TBA*), ulianzishwa mwaka 2002 kupitia Sheria ya Wakala Namba 30 ya mwaka 1997. Lengo la kuanzishwa *TBA* ni kutoa huduma bora na ya gharama nafuu ya makazi kwa watumishi wa umma na ofisi kwa Serikali na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufanuzi huu, naomba sasa, nitoe jibu swali la Mheshimiwa Dokta Maua Abeid Daftari, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, *TBA* inawajibika kuwajali wateja wake wakati wote na si pale tu wanapoibiwa. Wakala umekuwa ukishughulikia malalamiko na kero za wateja kila zinapojitokeza. Mfano, *TBA* imeanza ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba zote za viongozi eneo la Masaki, ili kuepusha uwezekano wa wakazi wa nyumba husika kuibowi. Aidha, katika kuwajali wateja wake, *TBA* imeanza uboreshaji wa miundombinu, barabara na mifereji ya maji ya mvua katika makazi ya eneo la Kisasa, Dodoma, ili kuondoa tatizo la maji kujaa katika maeneo haya.

(b) Mheshimiwa Spika, *TBA* imekuwa ikishughulikia matatizo ya wizi kwenye nyumba zake kwa kuhusisha vyombo vyaya usalama. Pale inapobainika kuwa wahusika wa wizi ni waajiriwa wa *TBA*, Wakala huwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria zilizopo, ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha au kuwafukuza kazi.

(c) Mheshimiwa Spika, *TBA* na *National Housing*, ni taasisi zenye majukumu tofauti. *TBA* imeanzishwa kwa lengo la kujenga na kutengeneza nyumba na majengo ya Ofisi za Serikali na Taasisi za Umma na kuwapatia Watumishi wa Umma huduma ya makazi bora na ya gharama nafuu wakati wakiwa kazini na baada ya kustaafu. Shirika la Nyumba la Taifa (*NHC*), linapangisha na kuuza nyumba zake kwa watu wote. Kwa maana hii, hakuna mwananchi, awe anafanya kazi ya umma au kazi nyingine, anayezuiliwa kutumia huduma za *NHC* pale zinapopatikana.

MHE. DKT. MAUA A. DFTARI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri, kwa majibu yake, lakini nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa mvua zimeanza Dodoma na baadhi ya nyumba zetu nyingi zinavuja. Ni ile ile kusema kwamba, *TBA* inapaswa kuwajali wateja wake, lakini hilo bado halijafanywa. Majumba yetu yote yanavuja, mapanya yapo ndani na *board* zote zinaloa zina mipaka na mito mbalimbali juu. Hata kule Kisasa kwa Waheshimiwa Wabunge wanakokaa, *fancing* haijatiwa.

Mheshimiwa Spika, je, Mheshimiwa Waziri ananiambiaje? Ni lini shughuli hii itashughulikiwa ipasavyo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakiri kwamba, kama nyumba zinavuja ni jukumu la *TBA* kuzifanyia matengenezo, kwa hiyo, kazi hiyo, tutakwenda kuishughulikia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kuhusu uzio katika nyumba za Kisasa, hiyo, tumeiweka kwenye mpango; tutafanyia kazi na tutajenga uzio kwenye nyumba zile za kisasa.

SPIKA: Utajuaje nyumba zinazovuja? Maana hujauliza ziko wapi?

Mheshimiwa Shekifu, swali la nyongeza?

MHE. HENRY D. SHEKIFU: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Waziri. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, kazi ya msingi ya *TBA*, ilikuwa ni kuhudumia sekta ya Serikali. Lakini kwa sasa *TBA* imejingiza katika biashara, kupangisha na kuuza nyumba, matokeo yake wameondoka kwenye wajibu wa msingi na matatizo makubwa yameanza kujitokeza. Hivyo, ni kwa nini *TBA* wasirudi katika kazi yao za msingi, kuhudumia shughuli za Serikali badala ya kwenda kuuza na kufanya biashara ya nyumba?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli katika majukumu ya *TBA* kwanza ni kujenga nyumba za kuishi, kujenga nyumba za Serikali, maofisi na pia kwa sababu wanatakiwa wapate fedha za kuweza kuhudumia nyumba hizi, kazi yao nyingine ni kupangisha. Kwa hiyo, siyo kwamba wameondoka kwenye jukumu lao la msingi, ni sehemu ya kuweza ku-*generate funds*, kutengeneza fedha ili kusudi waweze kuzihudumia nyumba hizi, makazi yawe bora zaidi, kwa hiyo, ni jukumu lao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kusimamia ili sehemu ile ya huduma kwa nyumba za Serikali iwe inatiliwa mkazo na sehemu ya kupangisha iwe ni sehemu tu ya kuongeza angalau wapate fedha za kuweza kujindesha.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Upatikanaji wa Dawa za Magonjwa Nyemelezi

MHE. RIZIKI S. LULIDA (K.n.y. MARGARETH A. MKANGA) aliuliza:-

Makali ya Ugonjwa wa UKIMWI huzidishwa na magonjwa nyemelezi kama vile *TB*, kisonono, malaria na kadhalika.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha kuwa dawa za kutibu magonjwa hayo zinapatikana kwa wingi katika Zahanati na Vituo vya Afya nchini?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imechukua hatua mbalimbali katika kukabiliana na upungufu wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika Vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza dawa za magonjwa nyemelezi.

Mheshimiwa Spika, dawa nyingi zinazotumika katika kukabiliana na magonjwa nyemelezi kwa watu wenyе virusi vya Ukimwi ni mionganoni mwa dawa zilizomo kwenye orodha ya dawa muhimu yaani *essential medicines list* zinazopatikana katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa umma nchini. Mfano wa dawa hizi ni pamoja na dawa aina ya *Seprine* inayotumika kukabiliana na ugonjwa wa homa ya mapafu yaani (*pneumocystis jiroveci pneumonia*), dawa aina ya *Fluconazole* inayotumika kutibu kuvu ambayo ni *fungus* na baadhi ya dawa aina ya *antibiotics* kama vile *Amoxicillin* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, dawa kwa ajili ya magonjwa kama kifua kikuu, malaria na kisonono zinapatikana bila malipo kwa watu wenyе virusi vya Ukimwi katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya umma na badhi ya vituo binafsi vilivyo dhinishwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa dawa hizi za magonjwa nyemelezi zinapatikana kwa wingi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma, Wizara kuititia Mpango wa Taifa wa kudhibiti Ukimwi hutenga fungu maalum kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa ajili ya kununulia dawa za magonjwa nyemelezi kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua fursa hii kuititia Bunge lako Tukufu kuwashukuru wadau wetu wote katika mapambano dhidi ya Ukimwi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya katika kuhakikisha dawa za magonjwa nyemelezi zinapatikana na kufika katika vituo husika.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna Taasisi mbalimbali mfano; *Global Fund, Basket Fund, Bill Clinton Foundation, George Bush Foundation* na Mashirika mbalimbali ikiwemo *TAC/AIDS* wanatoa fund nyingi kupeleka katika Halmashauri kusaidia kutibu magonjwa hayo nyemelezi lakini kinachosikitisha hizo fund hazitumiki vizuri.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inasimamia kwa makini kuhakikisha dawa na hizo pesa zinatumika kikamilifu katika Halmashauri zetu?

(b)Kuna *fund* inatolewa kwa ajili ya malaria lakini tukienda kuangalia vitabu mbalimbali vya Halmashauri hatuzioni, hizo fedha zinakwenda wapi? Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kutueleza hizo hela za malaria zinakwenda wapi? Ahsante.

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba fedha zinazotolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa hazi pelekwi katika Halmashauri, fedha hizi zinapelekwa *MSD*, *MSD* ndiyo wenyewe jukumu la kununua dawa hizi na kuzisambaza katika vituo husika. Kwa hiyo, Halmashauri hawapokei fedha kwa ajili ya dawa.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kuhusu mpango wa malaria, vilevile fedha zinazotolewa na wahisani wote ikiwemo *Global Fund*, *Basket Fund* na kadhalika, zinapelekwa katika mradi wa *Malaria Control Program* ambao wao ndiyo wenyewe jukumu la kuhakikisha kwamba *interventions* zote zile zilizopangwa kwa ajili ya kukabiliana na malaria wanazifanyia kazi husika kwa kushirikiana na wadau wengine mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa ufupi niseme tu kwamba fedha hizi zina maeneo maalum zinapokwenda na wala siyo kwenye Halmashauri moja kwa moja na kwa taarifa tulizokuwa nazo sasa ni kwamba fedha hizi zimekuwa zikitumika vizuri na mfano mzuri ni mafanikio yaliyopatikana katika mradi wa malaria ambapo vyandarua vimenunuliwa kwa wingi, dawa za kunyunuzia ndani ya nyumba zinatolewa, akina mama wanapata zile dawa za kujikinga wakati wa ujauzito na kadhalika jambo ambalo limepelekeea kupungua kwa maambukizi ya malaria kwa asilimia kubwa kutoka 18% mpaka 10% hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani mradi huu unakwenda vizuri na bila shaka tukiendelea kwa kasi hii, tuna matumaini ya kuweza kuondoa kabisa ugonjwa wa malaria nchini.

SPIKA: Ahsante, tunaendelea na swali linalofuata, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 12

Tatizo la Mawasiliano ya Simu Kata za Wilaya ya Uvinza

MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. DAVID Z. KAFULILA) aliuliza:-

Kwa muda mrefu Kata za Kyala, Mtegowanoti, Sunuka na Sigunga ndani ya Wilaya mpya ya Uvinza zinakabiliwa na tatizo la mawasiliano ya simu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzipa kipaumbele Kata hizo ili kuwaondoa wakazi hao katika maisha ya ujima?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mbunge wa Kigoma Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote (*UCAF*), tayari imepata kampuni ya kupeleka mawasiliano katika kata za Sunuka na Sigunga katika Wilaya mpya ya Uvinza. Tayari tumetenga ruzuku ya Dola za Kimarekani 245,000 kwa ajili hiyo. Kazi hii inatarajia kuanza kabla ya mwisho wa mwezi wa tatu.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge tulishaleta orodha ya vijiji na kata ambazo hazina mitandao ya simu, kwa nini Serikali isituletee mpango kazi wake ili tusiendelee kuuliza maswali ya namna hii?

(b) Katika swali ya msingi zimeulizwa kata nne lakini Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kata mbili, sasa ni lini hizi kata mbili nazo zitapatiwa mawasiliano ya simu ikiwa ni pamoja na kata nane za Wilaya ya Kibondo ambazo simu hazishiki kabisa?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nadhani inapendeza kwa wananchi kuona Wabunge wao wanauliza kuhusu matatizo ya maeneo yao, kama Mheshimiwa Mbunge atataka tumpe orodha ili asiulize tena na wananchi wasijue kama anauliza, tunaweza kufanya hivyo vilevile lakini maana yake ni kwamba mtafuta maswali yote yanayohusiana na masuala ya mawasiliano, nadhani si jambo jema. Nadhani ni vyema wananchi wakaona mnauliza na mnafuatilia lakini ushauri tumeupokea kwamba tutatoa orodha kwa awamu kadiri tunavyopeleka mawasiliano katika maeneo ambayo hayana mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kata hizi nyingine mbili ambazo sijazijibu ni kwamba katika awamu hii ya sasa bado tunaanza awamu nyingine ya kutangaza maeneo mapya, kuanzia mwezi wa pili tutatoa tenda, tutatangaza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ambacho ninataka kusema ni kwamba naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge tena kama nilivyofanya mwaka jana kwamba kila eneo ambalo halina mawasiliano nchini litapata mawasiliano ya simu kabla ya mwaka 2015, ndio ahadi ya chama chetu na tutaitekeleza.

SPIKA: Tuendelee na swali linalofuata.

Na. 13

Kuweka Minara ya Mawasiliano – Manyovu

MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. ALBERT O. NTABALIBA) aliuliza:-

Mawasiliano ni muhimu kibiashara, ulinzi na ustawi wa jamii:-

(a) Je, ni lini tarafa ya Muyama Jimboni Manyovu itawekewa mnara wa mawasiliano?

(b) Je, Serikali ipo tayari kufika Manyovu kuona hali ilivyo kwa kulinganisha minara mingi iliyopo upande wa Burundi wakati upande wa Tanzania hakuna minara?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote, tayari tumeshachagua kampuni ya simu itakayopeleka mawasiliano kwenye tarafa ya Muyama kama aliyouliza Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba. Tumetenga ruzuku ya dola za Kimarekani 173,000. Kwa ajili hiyo tunatarajia kazi hii itaanza kabla ya mwezi wa tatu mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, sehemu (b), Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba aliuliza kwamba je, Serikali ipo tayari kufika Manyovu kuona hali ilivyo na kulinganisha minara mingi iliyopo upande wa Burundi wakati Tanzania hakuna minara? Kwa niaba ya Serikali nitakuwa tayari kwenda kwenye Jimbo la Manyovu lakini siyo kushangaa minara iliyopo upande wa Burundi bali kuzindua mnara mpya ambao tutaujenga kabla ya mwisho wa mwezi wa tatu.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, toka tunaanzisha *UCAF*, kwa kweli kila mwaka imekuwa tuko kwenye utaratibu, tunafanya upembizi yakinifu, tunafanya *procurement* mpaka sasa hakuna hata mnara mmoja umewekwa na *UCAF* lakini wote ni mashahidi, wenyewe makampuni ya simu wamefanya kazi kubwa sana kupeleka mawasiliano vijiji. Kwa nini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri asituambie hapa, Serikali pamoja na kusubiri habari ya *UCAF* ina mkakati gani wa kuwaomba wenyewe makampuni ya simu ama kuwalazimisha waende kwenye maeneo hayo yote ya vijiji ambayo kwa kweli mengine yana biashara kubwa kama hili la Muyama ambalo ni mpakani na kuna wafanya biashara wengi?

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba hapa Bungeni tulipitisha Sheria ya Kuanzisha Mfuko wa *UCAF* mwaka 2006 lakini mfuko rasmi uliana mwaka 2009 baada ya kanuni kuandikwa na baada ya fedha kupatikana. Tumekuwa katika nyakati za majoribio kwa maana ya mfumo gani sahihi kwa kutoa ruzuku kwa ajili ya kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge yuko sahihi, tumechelewa lakini sasa safari hii ndiyo mara ya kwanza ambapo tenda zimetolewa na makampuni yamekubali, yamepewa kazi hiyo. Kwa mfano, eneo la Mheshimiwa Kafulila, tunaweza kutaja ni *Airtel* ambao wameshinda tenda ya kupeleka mawasiliano kwenye eneo hilo na yako maeneo mengi tu ya Waheshimiwa Wabunge ambayo tuta-share hiyo *information*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, safari hii tumefanya na Waheshimiwa Wabunge wataona kwa mara ya kwanza sasa makampuni yamepewa maeneo mahsus ya kupeleka mawasiliano. Kwa hiyo, safari hii siyo *story* tena kama ilivyokuwa huko nyuma na tunaamini kwamba, tutapata fedha za ziada na kwenye bajeti itakayokuja, tunategemea Waheshimiwa Wabunge mtakubali kwamba tupate fedha za ziada kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa makampuni kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ambayo hayana mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ya swal, ni kweli kwamba pamoja na jitihada hizi za *UCAF*, bado makampuni haya yanao wajibu wa kupanua biashara zao na kupeleka mawasiliano kule ambapo hakuna kama mkakati wa kibiashara. Tulipotoa leseni ya mawasiliano, mwanzo hatukutoa masharti kwamba waende maeneo yote, leseni ilitolewa kwa nchi nzima na makampuni yalikuwa yanachagua yaanze wapi na yaishie wapi, lakini ni dhahiri kwamba, makampuni mengi yalikimbilia mijini na ushindani wa kibiashara umekuwa kwenye kushusha bei, zaidi ya kupanua eneo la wateja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunajadiliana na ninapenda niseme kabisa kwamba, Serikali sasa itaanza kutafakari kama kuna haja ya kuwanyang'anya masafa makampuni ya simu maana masafa ni rasilimali na kampuni inapewa masafa kupeleka mawasiliano nchi nzima, kama tutabaini kwamba wenzetu hawa hawana dhamira ya kupeleka mawasiliano kote, tutafikiria namma ya kutumia wanasema *carrot and stick*. Hii UCAF ni ruzuku, ni *carrot*, lakini tunaruhusiwa kabisa kisheria kumpunguzia mtu masafa kule ambako hataki kupeleka mawasiliano na kunahitajika mawasiliano. Kwa hiyo, kuna vitu tunazungumza ndani ya Serikali, tunafikiria *devices*, njia za kuweza kuyalazimisha makampuni haya kupeleka mawasiliano kule ambako hakuna lakini pamoja na jithada hizi tunaongea na makampuni kwa mfano *Airtel* na *Vodacom*, wana mipango yao wenyewe ya kupanua mawasiliano kule ambako hakuna.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie tu kwa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba, nia ya Serikali hii ni kupeleka mawasiliano kote ambako hakuna mawasiliano kabla ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wamechomewa nyumba zao na wamechomewa mali zao na ninaamini kwamba, busara iliyotumika kuunda nchi yetu ni kubwa zaidi kuliko vitu vinavyotugawa sasa.

Na. 14

**Kuongeza Ruzuku Hospitali ya Jeshi ya
Ali Khamis Camp - Chakechake**

MHE. RUKIA KASSIM AHMED aliuliza:-

Hospitali ya Jeshi ya *Ali Khamis Camp*, Chakechake, iliyojengwa kwa ajili ya kuwahudumia Wanajeshi na familia zao, inahudumia idadi kubwa ya wananchi kwa sasa:-

Je, Serikali, haioni kwamba, ipo haja ya kuiongezea ruzuku ili iweze kuwahudumia vizuri wagonjwa wote wanaofika hospitalini hapo?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Serikali kwa ujumla haina pingamizi lolote kuiongezea ruzuku Hospitali ya *Ali Khamis Camp*, Chakechake. Hapana shaka iwapo hali ya fedha itakuwa nzuri Hospitali hiyo itaongezewa ruzuku. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Hospitali ya *Ali Khamis Camp*, imefanyiwa ukarabati mkubwa hivi karibuni ili kutekeleza ushauri alioutoa Mheshimiwa Mbunge Rukia Kassim Ahmed.

MHE. RUKIA KASSIM AHMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu mazuri aliyonipa, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ukarabati mkubwa umefanyiwa katika Hospitali hii na kwa kuwa, kuwa na jengo zuri la Hospitali, sio kuwa na huduma nzuri. Je, Mheshimiwa Waziri,

utaliahidi Bunge hili kuwa, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, Hospitali hii itaongezewa ruzuku pamoja na kupatiwa vifaa ambapo itaonekana kuwa ni Hospitali iliyo na hadhi nzuri?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa, Hospitali hii inahudumia raia wengi sana na kwa kuwa, raia hawa walikuwa wahudumiwe katika Hospitali za *SMZ*, je, kuna msaada wowote kutoka katika Wizara ya Afya Zanzibar kwenda katika Hospitali hii ya Jeshi?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, ni kweli, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ukarabati wa majengo ya Hospitali peke yake hayatoshi katika kutoa huduma zilizo bora za afya lakini kama nilivyosema ni kwamba, kweli Serikali, inahitaji kutoa vifaa bora vya tiba.

Mheshimiwa Spika, ameuliza je, tunao mpango wowote katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014 ya kutekeleza jambo hilo? Naomba tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyosema katika jibu langu la awali kwamba, tutaangalia hali ya fedha itakavyokuwa na *inshallah*, kama hali ya fedha itaruhusu, hapana shaka tutajitahidi kadiri inavyowezekana kutenga fedha, ili tuweze kupata vifaa bora, ili tuweze kuwashudumia wananchi wa Chakechake pamoja na maeneo mbalimbali ya Pemba kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kweli Hospitali ya *Ali Khamis* ipo Pemba na inaendeshwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Wizara ya Ulinzi lakini ni ukweli uliopo vilevile kwamba, Hospitali hii iko Pemba au iko kwa upande wa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi nayo inapaswa kutoa kitu chochote ili kutoa huduma hizo lakini mpaka sasa hakuna ruzuku au fedha zozote zinazotolewa ili kuunga mkono juhudhi ambazo zinachukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuititia Wizara yake ya Ulinzi. Lakini mimi namfahamu sana Mheshimiwa Mbunge Rukia Ahmed, ni mtu ambaye ana ushawishi mkubwa sana wa kuwashawishi watu kufanya mambo mazuri, namwomba tu ashirikiane nami ili kuishawishi Wizara ya Afya ya Zanzibar ili iweze kutoa chochote ili kutuunga mkono.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda umeisha kwa kweli, Hospitali yenyewe moja tu.

Sasa naomba kwanza niwatambue baadhi ya wageni tulionao hapa ndani. Tunao wageni walioko katika ukumbi wa Spika, naona protokoli itakuwa imizingatiwa, kuna Ndugu Gabriel Nderumaki huyu ni Kaimu Mhariri Mtendaji wa magazeti ya Serikali ya *Daily News*, *Sunday News* na Habari leo sijui yuko wapi, ahsante. (*Makof*)

Tuna Ndugu Ichikael Maro, huyu ni Mhariri wa magazeti ya Serikali *Sunday News* na *Daily News* na Habari Leo na yeze pia asimame. Ahsante sana Ndugu Maro, hii Ndugu haijulikani kama ni *gender* gani basi ndiyo hivyo hivyo. (*Makof*)

Halafu kuna Ndugu Vicky Mwambola, huyu ni Kaimu Meneja wa fedha magazeti ya Serikali. Ahsante sana, tunawataki kazi njema ya uandishi na kuhabarisha watu kwa mambo yaliyo sahihi. (*Makof*)

Kuna wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa January Makamba ambao wanatokea katika Taasisi inaitwa *Mboni Talk Show*. Sasa hawa, yuko *Mboni Masimba*, mtangazaji wa kipindi cha *Mboni Talk Show*. Yuko wapi sijui? Yuko ndugu George Tyson, mtayarishaji wa kipindi hicho, halafu yuko Sarah Kabilu kutoka *Mboni Talk Show*, yupo Said Mohamed kutoka *Mboni Talk Show* na yuko Stephan Milinga kutoka *Mboni Talk Show*. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa na ninyi mnaojua *Mboni Talk Show*, wamekuja hapa nadhani mta-talk kwelikweli leo, mimi sifahamu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyoona *Order Paper* ya leo, tukitoka hapa nitaomba Kamati ya Uongozi kwa maana ya Wenyeviti wa Kamati zote, tukutane kusudi tuweze kuangalia ratiba ya safari hii. Halafu jioni saa nane katika Ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote tutakaa pale kama utaratibu wetu wa kufanya *briefing* ya kila wakati. Sasa kwa sababu hiyo, Waheshimiwa Wabunge hiyo *briefing* pamoja na mambo yanayojitokeza na kwa sababu Bunge linakaa sasa hivi na mambo yanayojitokeza sehemu mbalimbali za nchi hususani maeneo ya Mtwara kidogo yanatia wasiwasi. Sasa kama ilivyo ada ya Dua letu sisi Wabunge, inabidi kuwa chombo cha kuleta amani, umoja. Sisi Wabunge tunapaswa kujadili mambo haya kwa busara kwa mujibu wa Dua yetu tunayofanya kila siku.

Sasa suala hili ni kubwa sana, najua kuna watu wameshaniletea vikaratasi hapa kwamba tulijadili kwa dharura, mimi nakubali lakini tukijadili kwa dharura hivi nyinyi wote mliosoma kwenye magazeti mnalielewa suala hili? Kwa hiyo, tumeona busara inatutuma kwamba tuunde Tume yetu sisi Wabunge, Tume hiyo itakwenda kuwasikiliza wale watu, tuwasikilize tu maana hata tukisema tuanze kuzungumza tunazungumza, sisi tunajua kitu gani? Tuwasikilize wenyewe na hapohapo tutaisikiliza Serikali, sasa hiyo Tume tukiunda tunataka kabla ya kumalizika Bunge hili tuweze kupata nafasi ya kuliongea humu ndani tukiwa na nguvu ya kuwa tunajua kinachoendelea.

Kwa hiyo, naombeni wote mliokuwa na kusudio la kulileta jambo hili tulijadili kwa kifungu cha 47, cha dharura, naomba tuelewane sisi ni watu wazima, sisi ni kiungo cha Taifa, sisi ni kiungo cha umoja wa Taifa hili, tulijadili hili suala kwa busara kusudi lipate muafaka wenyewe busara na hivyo ndivyo nitawaomba hata wenzetu wa Mtwara, ujumbe wangu utakapokwenda kule wawe tayari kuongea nao hasira zao, kilichopo waweze kuongea nao. Busara ya Duniani sasa hivi panapotokea mgogoro ni kuzungumza si vinginevyo. Kwa hiyo, tutawaomba waweze kuzungumza na Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa wamekwenda kule kama Tume. Sasa muundo wa Tume nitawatangazieni kwa wakati mzuri lakini watakwenda wakati wa kipindi hiki ili tuweze kupata taarifa kabla hatujaondoka.

Kwa hiyo, kutokana na hayo, naomba nihairishe kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 4.46 Asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,

Tarehe 30 Januari, 2013, Saa Tatu Asubuhi)